# HAKI ZAKO CHINI YA HAKI ZA KUJUA SHERIA ZA MASSACHUSETTS ZA WAFANYAKAZI WA MUDA

## Mashirika ya utumishi lazima yakupatie taarifa za msingi kuhusu kazi yako

Sheria inahitaji mashirika ya utumishi kukupa ilani kwa maandishi ikiwa na taarifa za msingi kuhusu kazi yoyote ambayo wanakutuma wewe kufanya. Hii inaitwa **Agizo la Kazi**. Una haki ya kuambia shirika la utumishi jinsi unavyotaka wakupatie agizo la kazi, kama vile kwa njia ya barua pepe, posta au kama unataka kuichukua wewe binafsi. Mashirika ya Utumishi LAZIMA yakupatie angalau taarifa zifuatazo:

- Jina, anwani na nambari ya simu ya: (i) shirika la utumishi; (ii) mtoa fidia ya wafanyakazi; (iii) mwajiri wa kituo cha kazi; na (iv) Idara ya Viwango vya Kazi (DLS).
- Maelezo ya kazi na iwapo nafasi hiyo itahitaji mavazi maaluma, vifaa, mafunzo na leseni;
- Siku ya malipo, kiwango cha malipo kwa saa, na kama malipo ya masaa ya nyongeza yanaweza kutokea;
- Tarehe ya kuanza, masaa ya kuanzia ya kila siku na saa unazotarajia kumaliza, na kama inajulikana, muda unaotarajiwa wa ajira;
- Ikiwa usafiri au chakula zitatolewa na shirika la utumishi au mwajiri wa kituo cha kazi;
- Malipo yoyote kutoka kwa mfanyakazi;
- Ikiwa kuna mgomo katika kituo cha kazi au kufungiwa nje kwa wafanyakazi; na
- Taarifa kwa lugha nyingi kuwa utaratibu wa kazi una taarifa muhimu kuhusu kazi hiyo, ajira, ushirika, zoezi la kazi, au kazi.

Shirika la utumishi linaweza kukupa taarifa ya kazi kwa simu, lakini ni LAZIMA wakutumie taarifa hiyo kwa maandishi KABLA ya mwisho wa kipindi cha kwanza cha malipo.

Uteuzi wako wa kazi ukibadilika, lazima shirika la utumishi likujulishe juu ya mabandiliko hayo kwa haraka mara tu wanapojua.

Ikiwa shirika la utumishi halitakupatia agizo la kazi na ungependa kufanya malalamiko dhidi ya shirika hilo la utumishi, tafadhali piga simu kwa Idara ya Viwango vya Kazi katika **(617) 626-6969**. Shirika la Utumishi haliwezi kukuwachisha kazi au kukupa kazi mbaya zaidi kwa sababu ulitoa malalamiko.

Kama unawekwa katika nafasi ya mtaalamu au kama katibu au Msaidizi wa Kiutawala si LAZIMA Shirika la Utumishi wakupe agizo la kazi.

## Shirika la utumishi na waajiri wa kituo cha kazi hawawezi kukulipisha ada kwa:

- Kujisajili na shirika la utumishi;
- Kukupa uteuzi wa kazi;
- Vipimo vya madawa ya kulevya, kadi za benki, kadi za kutoa fedha, hati za malipo au amri ya fedha;
- Kufanya uchunguzi wa rekodi za uhalifu za mkosaji za Massachusetts (CORI);
- Huduma za usafiri, kama matumizi ya huduma inahitajika; kama matumizi ya huduma za usafiri ni kwa hiari, ada huenda isizidi asilimia 3 ya mshahara wa kila siku au gharama halisi, yoyote iliyo ya kiwango cha chini;
- Bidhaa au huduma yoyote, ikiwa ni pamoja na usafiri, ambayo inaweza kusababisha wewe kulipwa chini ya kiwango cha chini cha mshahara wa Massachusetts;
- Shirika la Utumishi au mwajiri wa kituo cha kazi hawezi kukulazimisha kumnunulia bidhaa yoyote isipokuwa uwe unataka kununua.
- Tofauti na Haki za Wafanyakazi wa Muda Kujua Sheria, Sheria ya Mshahara ya Massachusetts kwa kijumla inakataza makubaliano ambayo mfanyakazi anawajibika kwa gharama za kawaida na za kibiashara za mwajiri. Matokeo yake, hakuna punguzo kwa mshahara inayoruhusiwa isipokuwa madhumuni yake iwe hasa kwa faida ya wafanyakazi (kama kwamba gharama iwe na thamani kubwa kwa wafanyakazi na anaweza kuitumia kwa uhuru bila kutegemea kazi aliyofanya.)

**Mashirika ya utumishi lazima warejeshe gharama yako ya usafiri iwapo watakutuma kwa kazi ambayo haipo.**
Hii si pamoja na gharama ya usafiri wa kupelekwa katika kituo cha kazi kwa ajili ya mahojiano ya kazi.

## Mashirika ya utumishi hayawezi:

- Kukupa habari za uongo, ulaghai au za kupotosha wakijua;
- Kukulazimisha kwenda kwa uteuzi ambao hautaki kwenda;
- Kuweka mali yako na kukataa kukurundishia;
- Kuweka ada ambayo walikulipisha kinyume cha sheria;
- Kukufuta kazi au kukupa kazi mbaya zaidi kwa sababu ulitekeleza haki zako chini ya sheria hii;
- Kukutuma kwa uteuzi wa kazi kufanya kazi ambayo ni kinyume cha sheria;
- Kutuma mtoto aliye chini ya umri kwa uteuzi wa kazi wakati anatakiwa kuwa shuleni;
- Kukutuma kwa uteuzi wa kazi ambapo leseni maalum inahitajika kama hauna leseni hiyo;
- Kukutuma kwenye kituo cha kazi ambapo kuna mgomo au kufungiwa nje kwa wafanyakazi bila kukujulisha.

**Kwa habari zaidi kuhusu Kujua Sheria au Kufanya Malalamiko kwa Wafanyakazi wa Muda, piga simu kwa Idara ya Viwango vya Kazi katika (617) 626-6969, au tembelea mass.gov/dols/epsap.** Sheria hii imetolewa na Idara ya Viwango vya Kazi (DLS) na kutekelezwa na Ofisi ya Mkuu wa Sheria, Kitengo cha Haki ya Kazi. Sheria hii inatumika kwa "mashirika ya utumishi" (yaani mashirika ya muda) kama inavyoelezwa na sheria.

**Ilani ya mahali pa kazi:** Ilani hii ya mahali pa kazi inakubaliana na masharti ya Sheria za Jumla za Massachusetts Sura ya 149, Sehemu ya 159C, ambayo inahitaji kuwa mashirika ya Utumishi waiweke mahali ambapo waombaji wa kazi na wafanyakazi wanaweza kutazama kwa urahisi.